# CHUO CHA HERMARGS

Mkuu wa Chuo cha HERMARGS chenye usajili Na. **REG/HAS/205** kilichopo Morogoro (Kinyenze - Kipera karibu na Chuo Kikuu Mzumbe) anayo furaha kuutangazia Umma nafasi za masomo katika ngazi za Astashahada na Stashahada (Certificate and Diploma levels) ya **Ustawi wa Jamii** (Social Work) na **Famasia** (Pharmacy and Pharmaceutical Science) yatakayoanza Oktoba, 2023 kwa **mwaka wa masomo 2023/2024**.

**Sifa za Mwombaji kwa Astashahada au Stashahada ya Famasia (Pharmacy and Pharmaceutical Sciences)**
Awe amehitimu Kidato cha Nne (Form IV) na kuwa na ufaulu wa kuanzia **alama D** katika masomo angalau manne (4) isipokuwa ya dini ambapo masomo mawili kati ya hayo yawe ni **Kemia na Baiolojia**.

**Sifa za Mwombaji kwa Astashahada au Stashahada ya Ustawi wa Jamii (Social Work)**
Awe amehitimu Kidato cha Nne (Form IV) na kuwa na ufaulu wa kuanzia alama D katika masomo manne (4) isipokuwa masomo ya DINI. Pia kwa Diploma awe mhitimu wa kidato cha sita (Form VI) na kuwa na ufaulu kuanzia alama E na S katika masomo MAWILI au kuwa na Cheti cha Ustawi wa Jamii au fani nyingine inayoendana.

## MUDA WA MASOMO KWA NGAZI ZA ASTASHAHADA NA STASHAHADA

1. Masomo kwa ajili ya Astashahada (Cheti/Certificate) yanasomwa kwa miaka miwili (NTA Level 4 & NTA Level 5) kwa Famasia na Mwaka mmoja kwa Ustawi wa Jamii.
2. Masomo kwa ajili ya Stashahada (Diploma) yasomwa kwa miaka mitatu (NTA Level 4, NTA Level 5 & NTA Level 6) au kwa Mtu aliye na Cheti atasoma Mwaka mmoja kwa Famasia na miaka miwili kwa Ustawi wa Jamii

## FOMU ZA KUJIUNGA

Kwa sasa kuna mfumo wa Udahili wa pamoja yaani **Central Admission System (CAS)** kwa Kada za Afya (Famasia) kupitia tovuti ya NACTVET www.nacte.go.tz kisha utabofya **Maombi ya Udahili Vyuo vya Afya** na fuata maelekezo. Kwa Ustawi wa Jamii (Social Work) maombi yatumwe chuoni. Kwa maelekezo zaidi wasiliana nasi:-

1. Ofisi ya Chuo kwa simu namba 0742 759 220, 0678 532 890 na 0787 047 650
2. Kwa Barua pepe ifuatayo: hermargs.institute@gmail.com
3. Pia tembelea Tovuti ya Chuo: www.hermargs.ac.tz

## MUDA WA KUTUMA MAOMBI

Muda wa kutuma maombi awamu ya kwanza ni kuanzia Tarehe **16 Mei, 2023** mpaka Tarehe **15 September, 2022**

## GHARAMA ZA KUTUMA MAOMBI NA NAMNA YA KULIPA

Gharama ya kutuma maombi kwa Ustawi wa Jamii ni **TSh. 30,000/=** yanapatikana pia kwenye fomu au Tovuti ya Chuo (**www.hermargs.ac.tz**) na Famasia ni **Tshs 10,000** kwa chuo kimoja na **Tshs 30,000** kwa vyuo zaidi ya kimoja.

## NAMNA YA KUTUMA MAOMBI

**Ustawi wa Jamii** watume maombi yao Chuoni na kwa **Famasia** watume kwa njia iliyoelekezwa hapo juu, pia unaweza kuwasiliana na Chuo ukasaidiwa kuomba NACTVET. Kwa FAMASIA ukiingia kwenye tovuti ya NACTVET na kubofya **Maombi ya Udahili Vyuo vya Afya** na fuata maelekezo ili kuchagua **Chuo cha HERMARGS** kinachopatikana **Morogoro** pamoja na kozi yako pendwa.

## GHARAMA ZA MASOMO CHUONI KWA MWAKA NA UTARATIBU WA MALIPO

Ada na michango yote kwa **Famasia** mwaka wa kwanza ni **TSh. 2,435,000/=** na **Ustawi wa Jamii** ada na michango ni TSh. **1,650,000**/= kwa mwaka. Ada hizi zinaweza lipwa kwa awamu zisizozidi nne.

**CHUO KINATOA HUDUMA YA MALAZI (HOSTELI) BURE KWA WANAFUNZI WOTE**

**KARIBUNI SANA**
**MKUU WA CHUO**